# Maswāli na Majibu

Powered By
INJILI MILELE

Oktoba 2, 2024

Mch. Almodad Amos Yaragwiller

Ep. 002

## MADA: UANA WA YESU

# Anaitwa “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?

### Utangulizi

Katika swali la kwanza tulilojifunza kuhusu habari ya uana wa Yesu, tuligundua kwamba kwa mujibu wa Zaburi 2:7 na Matendo 13:33, kitendo cha Baba kumzaa Mwana kilimaanisha kuwa siku moja Yesu angelifufuka kutoka kaburini. Na Yesu alipofufuka tu, Biblia inaandika kuwa ile ahadi ya Baba kumzaa Mwana ilitimia.

> **Zaburi 2:7 SUV**
> Nitaihubiri amri; BWANA aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.
>
> **Matendo 13:33 (SUV)**
> ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu **ahadi hiyo**, **kwa kumfufua Yesu**; kama ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili, Wewe ndiwe Mwanangu, mimi leo nimekuzaa.

Kwa mujibu wa Biblia hili Jina la Mwana lilianza wakati ahadi hiyo ya Kiunabii ilipotolewa, rejea .

> **Waebrania 1:5 SUV**
> Kwa maana alimwambia malaika yupi wakati wo wote, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa? Na tena Mimi nitakuwa kwake baba, Na yeye atakuwa kwangu mwana?

Ukipenda kurejea swali la kwanza kuhusu uana wa Yesu bofya hapa: EP. 001

## Matumizi ya jina “Mwana wa Mungu”

Yesu anayo majina mengi, lakini tunapomuita Mwana wa Mungu, tunarejea habari ya mpango mzima wa Yesu kufanyika mwanadamu, kwa kuutwaa mwili wa kibinadamu ili iwezekane kufa na pia iwezekane kufufuka, kwa sababu katika hali yake ya Uungu, kufa isingewezekana.

> **Wafilipi 2:7 SUV**
> bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;
>
> **Waebrania 2:9,17 SUV**
> ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aonje mauti kwa ajili ya kila mtu. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake.

Kwa ufupi, Jina la Yesu la “Mwana wa Mungu” linatupatia picha ya Yesu katika hali yake ya kujinyenyekeza, ambayo inamfanya aonekane katika hali ya Ubinadamu na aonekane mdogo na dhaifu zaidi, si tu kuliko Mungu Baba, bali pia mdogo kuliko hata malaika. Mada hii ya Nani mkubwa kati ya Yesu na Mungu Baba kutaijadili katika swali litakalofuata kwa undani zaidi.

## Matumizi ya Jina “Mungu Mwana”

Wakristo wengi wanaojifunza habari za mahusiano yaliyopo kati ya Mwana na Baba, hawapendi kumuita Yesu kwa kutumia jina “Mungu Mwana,” kwa sababu jina hili linaichora picha ya Yesu kama mowajapo ya Nafsi za Mungu. Kwa maneno mengine, mtu anapomtambua Yesu kama Mungu Mwana, anakua ametangaza kuwa kabla Yesu hajaitwa Mwana alikuwepo na alikua sawa na Baba.

Sasa hili ni jambo linalopingwa vikali kabisa kwa sababu kulikubali ni kukukubaliana kujenga msingi wa Fundisho la Utatu Mtakatifu. Sasa wale ambao huwa wanapinga Fundisho hili la Utatu Mtakatifu, wakati huo huo wakiwa hawataki kuleta mabishano na migogoro ya kiimani Kanisani, huwa wanakwepa kabisa kutumia jina la Mungu Mwana, kwa kigezo kwamba jina hilo halipo kabisa katika Maandiko Matakatifu, na kwamba haifai kabisa tulitumie jina hilo. Na makanisa yanayofundisha Fundisho la Mungu Mwana, yameshutumwa vikali kwamba yanaingiza imani ambayo haipo katika Maandiko yaliyovuviwa na Mungu.

Hebu sasa tuiulize Biblia, Je, ni kweli kabisa kwamba hakuna aya zenye uvuvio zinazomtambulisha Yesu kama Mungu Mwana? Majibu ni kwamba andiko lipo.

## Wapi katika Maandiko kuna ufafanuzi wa matumizi ya jina "Mungu Mwana"?

> **Yohana 1:18 SUV**
> Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; **Mungu Mwana** pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.

Hebu tazama tafsiri nyingine kadhaa zinazowasilisha na kuweka wazi Usahihi wa matumizi ya jina "Mungu Mwana," kama moja ya majina mengi aliyonayo Yesu:

> No one has seen God at any time; the only **begotten God** who is in the bosom of the Father, He has explained Him.
> New American Standard Bible Jn 1:18.
>
> No one has seen God at any time; **the one and only, God**, the one who is in the bosom of the Father—that one has made him known.
> The Lexham English Bible Jn 1:18.
>
> "Hakuna mtu aliyemwona Mungu kamwe. **Mwana wa pekee aliye sawa na Mungu** ambaye ameungana na Baba, ndiye aliyetujulisha habari za Mungu."
> Biblia Habari Njema
>
> "Hakuna mtu yeyote aliyemwona Mungu wakati wowote, ila ni **Mungu Mwana** pekee, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha."
> Neno: Biblia Takatifu

Tunahitimisha kwa kusema, ni sahihi kabisa kulitumia kumuita au kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, lakini pia ni sahihi kabisa kumuita Mungu Mwana.

Asante kwa kusoma na kufuatilia makala hii, unaruhusiwa kuisambaza kwa wengine pia. Huduma hii inafanywa na Injili Milele, na hapa chini kuna Button ambayo unaweza kuibofya ili kutazama na kusikiliza Video nyingine nyingi zinazotengenezezwa na Injili Milele. Ikiwa unamaswali au mapendekezo kuhusu mada ambazo wakati ujao tuziandikie makala za namna hii tafadhali usisite kuwasilisha maswali na maoni yako kupitia namba za simu au barua pepe kama ifuatavyo:

Simu/WhatsApp: +255718 834 621
Barua Pepe: modaofhope4u@gmail.com
Tovuti: imeandikwa.adventistafrica.org

Bofya Hapa Kutazama Video ya Somo Hili

YouTube Injili Milele